

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE



SHULE YA SEKONDARI BARIKIWA,
S.L.P 186,
LIWALE.

KUMB.NA.LDC/BKSS/JI/2020/001.

10/12/2020.

JINA

LIWALE

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BARIKIWA MWAKA 2018

1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza Mwaka 2020 katika Shule ya Sekondari BARIKIWA . Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021, Wewe unatakiwa kuripoti hapa shuleni si zaidi ya siku 7 tangu shule kufunguliwa.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

a) SARE ZA SHULE

WASICHANA

1. Sketi mbili rangi ya kijani (**SKETI IVUKE MAGOTI**) MSHONO IWE RINDA ZA KAWAIDA NA ISIWE NA **UFITO**) mfano wa Kitambaa umeambatanishwa, nunua Kitambaa ulichowekewa na si vinginevyo.
2. Mashati 2 meupe mikono mifupi Tetron.
3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza, visiwe na visigizo virefu.
4. Soksi nyeupe Jozi mbili (2) au zaidi
5. Sketi mbili (2) nyeusi (Tetron) kwa ajili ya kazi za nje.
6. Fulana mbili (2) rangi ya Blue yenye nembo ya Shule kwa ajili ya masomo ya jioni na kazi za nje.
7. Hijabu inaruhusiwa kwa anayetaka tu ila siyo lazima, Mitandio hairuhusiwi. Vazi la Hijabu lishonwe kwa kuzingatia masharti yake sketi ndefu pana inayofika kwenye vifundo vya miguu, Nusu kanzu yenye mikono mirefu isiyobana mwili wala kuonyesha maumbile ya mwili.
8. Tracksuit rangi ya Blue kwa ajili ya Michezo.

WAVULANA

1. Suruali mbili za rangi ya Kijani upana wa suruali chini usipungue 16 (modo hazitakiwi) Mfano wa Kitambaa umeambatanishwa. Nunua kitambaa ulichowekea na si vinginevyo.
2. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi tetroni.
3. Soksi nyeupe Jozi mbili zu zaidi.
4. Tracksuit mbili za blue kwa ajili ya kazi za nje
5. Suruali nyeusi mbili kwa ajili ya michezo
6. Fulana mbili rangi ya blue bahari zenye nembo ya Shule kwa ajili ya masomo ya jioni na kazi za nje (Muuzaji anauza Tsh 12,000 kila moja
7. Viatu vyeusi vya ngozi, vya kutumbukiza, visiwe na visigino virefu.
8. Mkanda mweusi uvaliwe na sururuli.

b) VIFAA VYA MASOMO DARASANI

- i. Madaftari 10 au zaidi Makubwa (Counter book)
- ii. Kalamu (Peni na Penseli)
- iii. Mkebe wa hesabu na rula
- iv. Kamusi ya Kiingereza na Kiswahili.
- v. Calculator (Kikokotozi) kwa ajili ya masomo ya hesabu na Sayansi.

c) WANAFUNZI WA HOSTELI

Wanafunzi wanaotoka mbali na shule na wanafunzi wote wa kike wanashauriwa kukaa hosteli. Shule itawezesha chumba, Wazazi wanatakiwa kuwezesha chakula, Mpishi, Afya, Maji, Sabuni na Mafuta ya Kupakaa.

d) VIFAA VYA USAFI

- i. Ndoo ndogo ya maji
- ii. Panga moja
- iii. Jembe moja.

e) CHAKULA

Wanafunzi wote wanatakiwa wapate chakula cha mchana shuleni, hivyo wazazi wanatakiwa kuchangia chakula na gharama ya mpishi.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995.

Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais –Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wanafunzi wote.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya Jioni (Preparation)
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya juu kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Uanafuzi katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa Mwili, Mavazi na mazingira ya shule
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali za Umma.

2.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- a. Wizi
- b. Uasherati, ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile Uvutaji wa bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na Kadhalika
- e. Kupigana au kupiga
- f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g. Kudharau bendera ya taifa
- h. Kuoja au kuolewa
- i. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga Amani na usalama wa watu.
- l. Kumiliki simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- a. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali (Fomu hii itakabidhishwa kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni)
- b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na Mkatiba wa kutoshiriki katika Migomo, Fujo na makosa ya jinai.
- c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanunu na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

NB: Uharibifu wowote wa makusudi kwa mali za shule kama vile majengo, samani, vitabu, kompyuta n.k utaofanywa na mwanafunzi hapa shule, mzazi na mtoto watawajibika kulipia gharama za uharibifu huo.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/ Maigizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA

.....
SALUMU S. KIMBENDERA
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BARIKIWA

KIAMBATANASHO NO. 1

A: TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI NA MKATABA

Mimi (jina) wa (mahali)

Nakubali kujiunga kidato cha kwanza shule ya sekondari **Barikiwa**, Naahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na sitashiriki katika migomo, fujo, utoro na makosa ya jinai.

Ninakubali kuadhibiwa pale nitakapostahili.

SAHIHI

TAREHE

B: TAMKO LA MZAZI/MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUSOMESHA

Mimi (jina) wa(mahali)

Ambaye ni mzazi/ mlezi wa (jina la mwanafunzi)

Nakubali kutimiza wajibu wangu wa kusomesha mtoto wangu kwa kumpatia mahitaji muhimu kama vile sare za shule, viatu, kalamu, madaftari, chakula pamoja na kumuhimiza kufika shuleni kama sheria za nchi zinavyoelekeza. Ninakubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yaliyotolewa na yatayotolewa na shule. Kazi yangu ni

SAHIHI

TAREHE

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**



BARIKIWA SEKONDARI SCHOOL,
P.O BOX 186,
LIWALE.
DECEMBER, 2020.

KUMB.NA.LDC/BKSS/JI/2020/002

THE MEDICAL OFFICER,
LIWALE DISTRICT HOSPITAL,
P.O BOX 179 ,
LIWALE.

REF.....

Please examine the above named person and certify his/her physical and mental fitness for being a student. Attention should be paid to the followings categories:

1. Eye (sight)
2. Hearing
3. Limbs
4. Speech
5. Leprosy
6. Epilepsy
7. Neurosis
8. Pregnancy
9. Sexual transmitted diseases
10. Other serious diseases

Yours faithfully

.....
KIMBENDERA S.S

HEAD MASTER

medical certificate (To be completed by government medical officer authorized medical personnel))

I have examined the above named person and I hereby certify that findings above are correct and that the person is fit/unfit to undergo secondary studies.

.....
SIGNATURE/ OFFICIAL STAMP

.....
DATE